TANGAZO LA SERIKALI Na. 868 la larehe. 18/10/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA USAFI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA YA MWAKA 2024

Jina

TS. Na. 223 la 2024

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Usafi na Uhifadhi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ya Mwaka 2024, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Usafi na Uhifadhi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ya Mwaka 2024, ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Mpangilio wa namba

**2**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa-
(a) kuyafanya maudhui yanayohusiana na tafsiri kuwa kanuni ya 3; na
(b) kufuta kanuni ya 3.

Marekebisho ya kanuni ya 3

**3.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 3 kama ilivyopangwa kwa kuongeza maneno "na Mkurugenzi" mara baada ya neno "atakayeteuliwa" katika tafsiri ya neno "Afisa Mwidhiniwa".

Marekebisho ya Jedwali la Tatu

**4**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Tatu kwa kufuta neno "ujazo" popote linapotokea na badala yake kuweka neno "uzito".

Dodoma,
29 Agosti, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi -OR-Tamisemi*